



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA DIWANI WA VITI  
MAALUM KUPITIA CHAMA CHA NCCR-MAGEUZI**

**Dodoma, 18 Februari, 2021**

Kifungu cha 35(1) (c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287, Kifungu cha 19 (1) (c) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, pamoja na Kifungu cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 vinaweka takwa la kuwa na Madiwani Wanawake wa Viti Maalum wasiopungua theluthi moja (1/3) ya Wajumbe wote wa Halmashauri husika.

Hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi hufanya uteuzi wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum katika Halmashauri zote nchini kwa kuzingatia ushindi wa chama husika. Katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020, Chama cha NCCR-Mageuzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kilipata Madiwani wawili (2).

Baada ya kupokea Fomu Namba 8E kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama cha NCCR-Mageuzi iliyowasilishwa kwa barua yenye Kumb. Na. NCCR-M/MM/TV/15/125 ya tarehe 5 Februari, 2021, Tume katika kikao chake cha tarehe 17 Februari, 2021 ilipitia na kukagua Fomu hiyo na baada ya kujiridhisha imemteua **Ndugu Renatha Lihange Mizungu** kuwa Diwani wa Viti Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi.

Imetolewa na:

  
Dkt. Wilson Mahera Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**